

Pambazuko

Toleo Namba 32

Jumatatu Machi 27 Aprili -2, 2023



Kamala Harris aja kufagilia Marekani

● *Anatarajiwa "kuizodoa" China*

Mchezaji apona kansa ya korodani

**Uk.
23**



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Bila Katiba bora, maendeleo ni ndoto

WANASIASA wengi, hasa ndani ya chama tawala, Chama Cha Mapinduzi bado wana mawazo mgando kwamba “wananchi waelimishwe kuhusu Katiba iliyopo na waelewe kabla ya kudai mpya.”

Hapa wanamaanisha kwamba wananchi wengi hawajui Katiba ya nchi yao - Tanzania. Je, ni kweli wananchi hawajui Katiba? Ni kigezo gani kinachoonesa kwamba wananchi wengi hawajui Katiba?

Watanzania na watu wengi duniani walishuhudia mchakato wa Katiba mpya (katiba ya Warioba) ambayo hata hivyo ilikwama baada ya wanasiasa kuuteka nyara mchakato ule.

Tulishudia Tume ya Katiba ikizunguka nchi nzima kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi katika “ujenzi” wa katiba mpya. Watu waliitikia kwa wingi kila mikutano ya tume ilipopita, wananchi walifanya kile walichotakiwa - yaani kutoa maoni yao ambayo yaliratibiwa vyema na hata kupatikana rasimu.

Swali linakuja, je, nani aliu mchatato ule? Ni wananchi wanaodaiwa kutokuwa na uelewa kuhusu Katiba au ni wanasiasa wanaojidai kuijua Katiba?

Kama wananchi walifanya sehemu yao; yaani kutoa maoni, utasemaje waelimishwe kuhusu Katiba badala ya wale walioharibu mchakato ule kwa kuyapindisha yale walivyotumwa na wananchi kwa kuweka mambo yao wenyewe?

Swali wanalojuliza watu wengi, ni kwanini linapoongelewa suala la Katiba (mpya) visingizio vya kukwamisha au kuchelewesha kutoka kwa “wanufaika” wa Katiba iliyopo vinakuwa vingi?

Inawezekana kauli ya kwamba

“kila mtu ana hamu ya Katiba mpya, lakini tutumie muda, watu waelewe kitu gani kinahitajika ndani yake.” inashangaza kusema kwamba kila mtu anahitaji Katiba mpya wakati ni juzi tu wanasiasa wetu walipiga kelele kwamba huu ni muda wa maendeleo, siyo wa Katiba!

Lakini pili, kwamba wananchi waelewe kitu gani kinatakiwa kwenye Katiba, kwani maoni yaliyochukuliwa na Jaji Joseph Warioba yalitoka wapi kama siyo kwa wananchi? Iweje leo hawajui tena kinachohitajika ndani ya katiba wakati walitoka maoni yao?

Tatu, nani huyo anayeamua kwamba mambo fulani ndiyo yanahitajika kwenye Katiba? Siyo wananchi wenyewe wanaotoa yale wanayoona yanafaa? Tunaanzaje kuwaambia kwamba kuna yasiyotakiwa katika Katiba? Nani ametoa hiyo “amri” ya kuamua mapeenzi au uamuzi wa Watanzania?

Mwalimu Nyerere aliwahi kusema; ili tuendelee tunahitahi watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Mungu alishatuumba sisi watu, hivyo hakuna shida ya watu maana tupo tele. Mungu pia alitupatia ardhi (na rasilimali zote) hivyo ardhi siyo tatizo maana ipo tele. Tatizo lipo kwenye uongozi bora na siasa safi, ili viwili hivyo viweze kuongoza watu kutumia rasilimali kuleta maendeleo.

Lakini, siasa safi na uongozi bora havina budi kutokana na Katiba bora. Bila mwongozo thabiti ambao umo katika Katiba bora, maendeleo tutaendelea kuyasikia!

Hivi sasa Katiba yetu ina ‘mashimo’ mengi mno yanayoweke vizingiti vikubwa kwa maendeleo yenyte kudumu kwa vizazi.

TULIKOTOKA...



Muasisi na Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, akimfariji mjane wa aliyekuwa Rais wa Msumbiji, Graca Simbine Machel, baada ya mumewe, Samora Machel kufariki dunia katika ajali ya ndege iliyotokea Oktoba 19, 1986. Mwalimu (sasa marehemu) alikwenda Msumbiji kushiriki msiba huo. (Picha kutoka Maktaba ya Pambazuko).

NUKUU



“Serikali inafanya kila linalowezekana kuwapa elimu, lakini uamuzi wa kuitumia elimu hiyo ni wenu, tambueni kuwa upo msigo mkubwa sana wa kuongoza hii nchi unawasubiri, someni kwa bidii sana, mpate maarifa na ufahamu mkubwa. Msituangushe” - Benjamin William Mkaapa, Rais wa Tanzania (1995 - 2005). Mkaapa sasa ni marehemu.

Tafakuri**Tunatokaje kwenye mkwamo huu?****Na Plato Hekimachus**

MARA baada ya kushika madaraka ya kuongoza nchi, Rais Samia Suluhu Hassan – kwa maneno yake aliyorudia mara kwa mara, kwamba “Tanzania ni yetu sote,” alionekana kurudisha imani ya wananchi kwamba sasa nchi inakwenda mahali pazuri.

Kauli hiyo ya Rais Samia, iliondoa ukakasi wa “umimi” uliokumbatiwa mno na utawala uliopita, chini ya aliyekuwa mkuu wa nchi, Rais John Pombe Magufuli ambaye aliaminisha wananchi kwamba wenye hati miliki ya Tanzania ni viongozi wakuu, hasa yeye binafsi na pengine wachache ndani ya chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wakati ule, Rais Magufuli hakuamini kama nje ya CCM au yeye binafsi, kuna mawazo mazuri ya kuisukuma nchi mbele, wala kusaidia kuondoa changamoto za idadi kubwa ya wananchi – hasa hali ya ufukara inayoonekana kwa wananchi wengi, siyo wa vijijini tu, bali hata maeneo ya mijini.

Rais Magufuli aliamua kuwatosa mbali viongozi wa vyama vya siasa, wanazuoni wenye mawazo mbadala, viongozi wa dini, wanaharakati waliokuwa na mawazo yenye kujenga na hata wananchi wa kawaida. Hawa wote aliamini hawawezi kusaidia nchi.

Hata hivyo, hayo yaliyoonekana kwa Magufuli, bado yapo, licha ya kwamba Rais Samia amelegeza kidogo kamba ambayo ilitumiwa na mtangulizi wake “kuwamaliza” kabisa watu wenye itikadi, mitazamo na mawazo tofauti na yeye.

Rais Samia tofauti na “jeuri” ya mtangulizi wake, hivi sasa anaweza kuwaalika Ikulu watu wenye itikadi, mawazo na mitazamo tofauti na yeye ama chama chake na kufanya mazungumzo yanayohusu nchi. Hata hivyo, wengi hatuna uhakika kama mawazo ya hao “wageni waalikwa” anayatumia.

Kuwaalika Ikulu ni jambo jema, lakini

*Rais Samia Suluhu Hassan*

ni jema zaidi ikiwa atatumia mawazo na ushauri bora wa wananchi hao wenye mitazamo tofauti kujenga nchi, badala ya kukumbatia watu walewale miaka nenda rudi katika nafasi za uongozi. Huenda mawazo yaleyale ndiyo yamelifikisha taifa katika mkwamo.

Hata kuwalipa mali na stahiki wapinzani ambao waliumizwa na utawala uliopita, bado haitoshi, kuwaondoa magerezani na mahabusu bado pia hakutoshi, kuwaambia “rudini nyumbani tujenge nchi” nako hakutoshi na hata wachache kuwapa dhamana ndani ya serikali, hakutoshi aslani!

Pengine sasa ni wakati muafaka kwa Rais Samia kuita watu wenye mawazo mbadala kujadili juu ya masuala mbalimbali ya nchi.

Mfano anaweza kuanza kualika watu kadhaa na kujadili kuhusu njia bora za kuhakikisha bidhaa na hasa vyakula havipandi bei kiholela, namna ya kupunguza rushwa na kukuza uwajibikaji kwa viongozi wa umma na zaidi sana.

Endapo ataalika watu wengi wenye maono na mitazamo mbadala, anaweza kabisa kupata njia nzuri za kuondoa kila kinachoonekana kuwa mkwamo.

Inawezekana.

Mashabiki wa ‘wabunge’ waparurana

Na Tryruckia MFINANGA

MNYUKANO wa kukusanya wafuasi, mashabiki na wapambe ili kujiandaa kwa kinyang’anyiro cha ubunge wa Jimbo la Iringa Mjini, sasa ni dhahiri.

Kwamba wanaoamini watapitishwa na vyama vyao kuwania kiti hicho kwenye uchaguzi ujao wa Novemba 2025, wameanza “kuonyeshana” umwamba hadharani.

Hao ni aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo kupitia Chadema, Peter Msigwa na wakilishi wa sasa wa wananchi bungeni, Jesca Msambatavangu. Msigwa alikuwa mbunge wa jimbo hilo kwa miaka 10 – kuanzia mwaka 2010 hadi 2020.

Tangu kuanza kwa mwaka huu, wale wanaojitanabaisha kuwa wapambe wa wanasiasa hao wamekuwa “wakitunishiana misuli” ya kukubalika kwa wanayemshabikia kila wanapokuwa kwenye vijive vya kahawa; kwenye maeneo ya shughuli zao, hasa stendi ya mabasi na vituo vya daladala.

Wafuasi na mashabiki wa Msigwa, wanaendelea kudai kwamba mbunge wa sasa, Msambatavangu hana ubavu wa kumshinda hata kama uchaguzi utaitishwa leo.

Wiki iliyopita, katika eneo la stendi ya mabasi, kundi la vijana waliibuka na kuanza kuzungumzia siasa za Iringa, huku wakieleza kwamba jimbo hilo bila mbunge kuwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) hakuna maendeleo yatakayoonekana.

“Mnakumbuka miaka 10 ya ubunge wa Msigwa, mlipata nini hapa, hakuna maendeleo yaliyoonekana, lakini sasa mnaona mji wetu unavyokimbia kwa maendeleo, hatuna shida ya maji wala umeme,” alisikika kijana mmoja akisema.

Mwingine akadakia, kuwa katika kipindi cha ubunge wa Msigwa, Iringa iligeuka uwa uwanja wa siasa, hakuna kazi za maendeleo zilizokuwa zikifanyika – kwania kuanzia mbunge hadi wananchi walikalia siasa.

Hata hivyo, kijana mwingine akisikika kuwa shabiki wa Msigwa alisema mbunge wa sasa aanze kuaga, kwani kwenye



Jesca Msambatavangu.

uchaguzi ujao, “hana chake.”

Hivi karibuni Msambatavangu alifanya ziara katika jimbo hilo na kukumbana na kadhia ya baadhi ya vijana ambao walioonekana kuvuruga ziara hiyo.

Ipo video iliyosambaa mitandaoni mwanzoni mwa wiki iliyopita ikionyesha baadhi ya vijana wakiimba kuwa hawamtaki mbunge wa sasa na kwamba wanamtaka mbunge wa zamani Peter Msigwa.

Akizungumzia video hiyo, Msambatavangu anasema hiyo ni sehemu ndogo ya vijana waliopangwa na wanasiasa ili kumchafua na wala siyo miongoni mwa vijana zaidi ya 1500 waliokuwa wakipewa maeneo yao eneo la Mlandege.

Msambatavangu anadai vijana walioonekana wakibeba utendaji kazi wake na kuwa hawamtaki ni makada wa Chadema ambao walipanga kuvuruga ziara yake.

Mbunge huyo pia amekanusha taarifa zilizosambaa mitandao ya kijamii kwamba katika ziara yake hiyo alirushiwa mchanga na ulazimika kuikatiza.

Mbunge amepongeza vijana wengi katika Manispaa ya Iringa kwa kuwa wavumilivu na kushiriki kwenye zoezi la kuwahamisha kutoka mbele ya maduka ya wafanyabiashara mjini humo kwenda eneo la Mlandege, eno lililotengwa kwa ajili ya biashara zao.

Habari

Eacop yathamini mila, yachepusha bomba

Na Scovya MANASE

KATIKA kuheshimu mila, desturi na tamaduni za makabila nchini Tanzania, Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (Eacop), imeamua kuchepusha mtandao wake kusafirisha mafuta.

Kutokana na hatua hiyo, sasa makaburi yaliyokuwa yakiguswa na mtandao wa bomba la kusafirisha mafuta hayo, katika Kijiji cha Mwamayoka, wilayani Igunga, Tabora, hayataguswa.

Wiki iliyopita, Eacop ilisaini mkataba wa makubaliano baina yake na wananchi wa kabila na jamii ya Wataturu wanaoishi katika hicho kwa ajili ya kuchepusha njia ili kuyalinda makaburi yao ya kimila.

Awali, ramani ya njia ya bomba hilo ilionyesha kwamba jamii ya Wataturu katika kijiji hicho, wataguswa – hasa makaburi yao ya kimila ambayo waliomba yasihamishwe.

Makaburi yao yaliyopo eneo la Bung'enda na maeneo yao mengine kadhaa ya kuabudia, sasa hayatahamishwa kupisha mradi huo mkubwa wa kukuza uchumi wa Tanzania.

Akizungumza wakati wa sherehe ya kusaini makubaliano hayo wiki iliyopita, Mkurugenzi Mkuu wa Eacop – Tanzania, Wendy Brown alisema baada ya majadiliano na jamii na viongozi wa kimila, Eacop ilifanya mapitio ya kiufundi na kukubali kupitisha bomba hilo katika njia mpya ili kutokuwa na athari yoyote katika maeneo yao muhimu ya mila na kiutamaduni.

Wendy alisema Eacop itaendelea kushirikiana na jamii zote zilizoguswa na mradi pamoja na viongozi wao wa kimila ili kuhakikisha kuwa maoni yao yamezingatiwa wakati wote wa kupanga na kutekeleza mradi.

Mkataba huu wa jamii huyo ni wa pili kusainiwa na EACOP baada ya kusaini mkataba kama huo hapo awali na jamii ya



Mkurugenzi Mkuu wa Eacop, Wendy Brown (katikati mwenye miwani) akisaini mkataba wa makubaliano baina ya kampuni yake na viongozi wa jamii ya Wataturu wilayani Igunga, Tabora wiki iliyopita. (Picha na Mpigapicha Wetu).

watu wa kabila la Akie inayoishi Kanda ya Kaskazini.

Kiongozi wa jamii ya Wataturu, Chifu Gesuda Masanja, alipongeza hatua ya Eacop kwa kujali mila zao, huku akielezea kuwa mradi huo utasaidia kwa maendeleo ya jamii yake.

Akizungumza awali, Martha Bayo, ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Igunga, pia alipongeza hatua ya Eacop na kuitaka jamii ya Wataturu kuwa walenzi wa bomba hilo la mafuta ghafi litakapokamilika.

Mmoja wa viongozi wa kutoka Jukwaa la Wafugaji – shirika lisilokuwa la Kiserikali (Pingos), Nailejileji Tipap alisema hatua ya kampuni ya Eacop kusaini mkataba huo ni kulinda haki, mila na desturi za jamii ya Wataturu.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Igunga, Godlove Kawiche akizungumza kwa niaba ya mkuu wa wilaya hiyo alisema serikali itahakikisha mradi huo unakamilika kama ulivyopangwa bila kuwepo kwa vikwazo kutoka kwa wananchi kwani tayari wanatambua manufaa ya kuwepo kwa mradi huo mkubwa wa kimkakati.

DCI aomba msamaha kwa uongo

**Na Mwandishi MAALUM
Nairobi, Kenya**

OFISI ya Mkurugenzi wa Kuchunguza Makosa ya Jinai (DCI) ya Kenya, imelazimika kuomba msamaha kwa umma baada ya kuchapisha picha ikidai zilipigwa wakati wa maandamano ya Machi 20, mwaka huu yaliyoitishwa na kiongozi wa upinzani nchini humo, Raila Odinga.

Picha hizo zinazoonyesha baadhi ya waandamaji wakifanya vurugu, zilisambazwa na ofisi hiyo kwenye mitandao ya kijamii.

Viongozi wa vyama vya upinzani ndani ya umoja maarufu wa Azimio la Umoja Kenya, Raila Odinga na Martha Karua, juzi – Jumamosi, waliitaka ofisi hiyo kuomba msamaha kwa Wakenya na dunia kwa kusambaza uongo.

“Hawa ni waongo, wamesambaza picha za zamani sana wakitaka kuaminisha umma kwamba maandamano tuliyoitisha yalikuwa ya vurugu,” alilalamika Raila.

Raila, ambaye aligombea urais, akichuana na rais wa sasa, William Ruto alisema ofisi ya DCI huenda ilifanya kazi hiyo ya uongo kwa maelekezo maalum ili ionekane Wakenya wanaopigana kupata maisha bora kupitia maandamano, ni wahuni na watu wa vurugu.

“Serikali yote ya Ruto inatambua haikupata ushindi na ndiyo maana haikubaliki, siyo kwa wafuasi wa vyama vya siasa pekee, bali idadi kubwa ya Wakenya hawakumchagua, sasa wanadai haki yao, lakini kubwa zaidi, serikali iliyoahidi kusaaidia kupunguza ukali wa maisha, imewageuka,” aling’aka Raila akiwa jijini Nairobi.

Kiongozi mwingine, Karua alisema - “Ofisi ya DCI haiwezi ikaaminika na haiwezi ikafanya uchunguzi huru baada ya kuanikwa na vyombo vya habari.”

Karua alisema kwa kutumia picha kwa nia oву, inaonekana serikali inapanga kutumia wahalifu kuvuruga maandamano yao yaliyoratibiwa kufanyika kesho -



Raila Odinga

Jumatatu, Machi 27, 2023.

Katika taarifa ya ofisi ya DCI iliyochapishwa kwenye ukurasa rasmi wa Twitter, ilieleza kughafirika katika kuchapisha picha hizo na kwamba haikuwa na nia oву yoyote.

Ofisi hiyo ilisema; “tulikuwa na picha nyingi sana za matukio hayo, sasa katika kuchapisha nadhani tulichanganya na matukio mengine kwa bahati mbaya.”

Taarifa hiyo iliyoendelea kueleza kuwa katika uchakataji na hata mfumo wa kutuma picha hizo, ikajitokeza mkanganyiko wa picha ambazo hazikuwa za tukio la maandamno ya Machi 20, 2023.

Ofisi hiyo iliendelea kuhimiza Wakenya wote wenye picha za watu walioonekana wakifanya vurugu wakati wa maandamano hayo, kutuma kwao, ili kuanza kwa uchunguzi haraka na ikithibitika kuna uvunjifu wa sheria, basi wahusika wakamatwe na kuhojiwa.

Gazeti la Taifa Leo la Kenya katika toleo lake la Jumamosi – Machi 25, 2023 lilianika jinsi Ofisi ya DCI ilivyozembea kutumia teknolojia na hata kubainika kuwa iliweka picha za matukio ya zamani.

Mada Murua

Ustawi na mgawanyiko wa mamlaka

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

HAIWEZEKANI kuzungumza juu ya umiliki wa taifa pasipo kuzungumzia mgawanyiko wa mamlaka.

Eleweke kuwa siasa katika nyakati hizi ni hasa juu ya mgawanyiko wa mamlaka ili kuwezesha utoaji haki na utoaji wa huduma muhimu kwa jamii.

Fikra za kisiasa au utendaji wa kisiasa, kwa kila wakati unapaswa kuzingatia na kuendana na namna ya uelewa juu ya haki ulivyojengeka na ufanisi wa mfumo mzima wa ustawi kwa ajili ya kuongeza ubora wa maisha ya raia.

Baada ya ukoloni, mataifa mengi yaliyopata uhuru 'yalikimbilia' kujenga miundo na mifumo mipya ya utawala ambayo ingeongeza haki na kuhakikisha ufanisi katika ujenzi wa ustawi wa watu.


Kiini cha juhudi hizo ilikuwa kudhihirisha kwa maneno na vitendo kwamba kuwa huru maana yake ni kuweka umiliki wa taifa na mamlaka mikononi mwa watu.

Hata hivyo, inasikitisha kwamba matokeo ya juhudi hizi hayajawa ya mafanikio katika nchi nyingi zilizokuwa chini ya ukoloni

Kwa uelewa huo wa mgawanyiko wa mamlaka kwa nyakati hizi - na bila shaka kwa nyakati zijazo, una malengo hayo. Kwa hiyo basi ni juu ya watawala siku zote kuweka sikio lao kwa jamii ambayo ndio wenye taifa na ndio wenye madaraka ili kujua ni nini jamii inahitaji kwa kila nyakati. Kwa serikali iliyo ya watu inayoongozwa kwa matakwa ya watu haiwezi kupuuzwa sauti za watu.

Mgawanyiko wa mamlaka ulio na ufanisi - mara zote, utakuwa na uwezo wa kubadilika na kubadilisha mambo kulingana na mahitaji ya jamii.

Viongozi wanapaswa kuwa na maono ya uongozi wao, lakini hayo yaweza kutekelezwa kwa mafanikio pale tu yanaporandana na matakwa ya watu.



Mwalim JK Nyerere

Kwa hiyo, kimsingi kulingana na nadharia hii, wanaoamua juu ya mwelekeo wa taifa ni watu na wala siyo watawala.

Hii ndio sababu bunge kama chombo kinachowakilisha watu, lina nafasi kubwa katika kudhihirisha dhamira ile kwamba mamlaka imo mikononi mwa watu.

Mabadiliko yanayoendana na kubadika kwa matakwa ya watu kulingana na nyakati yanakuja na mambo mengi. Miongoni mwa hayo ni mabadiliko ya sheria na wakati mwingine mabadiliko ya katiba ya nchi.

Suala la mabadiliko ya sheria na ikibidi mabadiliko ya katiba siyo matakwa au hiari ya watawala bali ya watu. Vilevile mabadiliko hayo yanaweza kudai mabadiliko ya watawala na kufumua miundo na mifumo ya utawala ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mambo kwa malengo ya kuboresha maisha ya watu.

Pale ulipo utawala bora suala la mabadiliko ya katiba na sheria kwa manufaa ya jamii siyo jambo la kuvutana, bali la kuunganisha watawala na watawaliwa katika safari ya kuboresha maisha ya jamii.

Mezani kwa Chahali



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Nini kitarajiwe ziara ya Harris?

BAADAYE wiki hii, Tanzania itapata Ugeni mkubwa, na wa kihistoria. Ugeni huo ni wa ujio wa Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris.

Ni ugeni wa kihistoria kwa sababu Harris siyo tu ni mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo huko Marekani, bali pia ni Mmarekani mweusi wa kwanza kushika nafasi hiyo.

Wakati ujio wa makamu huyo wa Rais wa Marekani ni habari njema, atazuru Tanzania wakati kuna vuguvugu kubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki dhidi ya ushoga.

Majuzi tu, Bunge la Uganda limepitisha sheria kali dhidi ya ushoga. Huko Kenya nako, japo Mahakama Kuu imetoa uamuzi unaoelemea kwenye haki za mashoga, serikali ya Rais William Ruto imeeleza bayana kuwa haitoruhusu ushoga nchini humo.

Unaweza kujiuliza “masuala ya ushoga na ujio wa Harris wapi na wapi?” Ni kwamba mwanasiasa huyo ni mmoja wa watetezi wakubwa wa haki za mashoga nchini Marekani.

Baadhi ya wafuatiliaji wa mambo wanasubiri kuona kama atazungumzia suala hilo atakapokuwa ziarani nchini Tanzania.

Japo harakati dhidi ya ushoga nchini Tanzania hazijafikia kiwango cha hali ilivyo nchini Uganda na Kenya, Tanzania imeshuhudia kuwepo kwa maandamano mawili, huko Mwanza na Arusha, yaliyoandaliwa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata) kupinga ushoga.

Kadhali, majuzi, Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango alikemea vikali vitendo vya ushoga, akieleza kuwa “hata wanyama hawafanyi mapenzi ya jinsia moja.”

“Hili ni gumu kweli, maadili ya nchi yetu yameporomoka sana, yaani na



Kamala Harris.

mengine hata kuyasema ni ngumu. Ndoa za wanaume wawili? Ndoa za wanawake wawili? Mlizonia wapi? Hata wanyama hawafanyi hivi,” alisema Dkt. Mpango.

Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa huko Marekani kuhusu ziara hiyo ya Harris barani Afrika, suala la haki za mashoga halikutajwa kuwa miongoni mwa vipaumbele vya kiongozi huyo.

Pamoja na kwamba upo uwezekano wa kuzungumzia suala hilo, hasa kwa kumuuliza Rais Samia Suluhu Hassan msimamo wa Tanzania katika suala hilo.

Ziara ya Harris inafanyika wakati makundi makubwa mawili ya imani yakiwa kwenye ibada muhimu zaidi; Wakristo wakiwa kwenye msimu wa Kwaresma na Waislamu wakiwa kwenye Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, hivyo upo uwezekano wa kiongozi huyo wa taifa kubwa kushauriwa na wasaidizi wake, hasa balozi wa nchi yake hapa Tanzania, kwamba ni vyema kuepuka kuzungumzia suala hilo.

Mwisho, ni matumaini yangu kuona ziara hiyo ya Makamu wa Rais wa Marekani ikileta matokeo mazuri kwa Tanzania hususan katika fursa za kiuchumi sambamba na sayansi na teknolojia, eneo ambalo Marekani imepiga hatua kubwa sana.

Habari

Kamala Harris aja kufagilia Marekani

Na Mwandishi WETU

TANZANIA ni miongoni mwa nchi chache za Afrika ambazo “zinatolewa macho” zaidi na mataifa makubwa mawili yenye uchumi imara na nguvu kubwa za kijeshi.

Mataifa hayo yanatamani na yako katika mikakati ya kuhakikisha yanakuwa karibu zaidi na nchi za Afrika ili kutimiza malengo yao; ya wazi na hata yenye kificho.

Mataifa hayo ni Marekani na China ambayo yamekuwa “yakigombea” kukubalika zaidi katika nchi za Afrika, kwa malengo tofauti, hata kama viongozi wa nchi hizo tajiri wanaeleza kuwa ni “kukuza ushirikiano wa kibiashara na kidugu.”

Katika kuhakikisha wanakuwa na uhusiano “mzuri” na Afrika, viongozi wakuu wa nchi hizo mbili wamekuwa wakipishana kufanya ziara katika ardhi ya nchi za Afrika ama kuwaalika viongozi wake New York, Marekani au Beijing, China kwa mazungumzo ya “kukuza ushirikiano.”

Jana, Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris alianza ziara ya siku tatu nchini Ghana ambako atakuwepo kwa siku tatu kabla ya kuanza safari ya saa zinazozidi nane kutoka Uwanja wa Kimataifa wa Kotoka, Accra hadi Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Dar es Salaam, Tanzania.

Kiongozi huyo nambari mbili kwa dhamana ya juu nchini Marekani, atawasili Dar es Salaam, Jumatano-Machi 29, 2023 kwa ziara ya siku tatu kabla ya kuelekea Lusaka, Zambia. Atarejea Marekani Aprili Mosi, 2023.

Ratiba ya kiongozi huyo inaonyesha kuwa atakutana na marais wa nchi hizo tatu na anapanga kutangaza fursa zaidi namna Marekani inavyoweza kushirikishwa “kukamua” madhila ya sekta za elimu, afya teknolojia na nishati.

Wachambuzi wa siasa na uchumi wanaeleza kwamba lengo kubwa la ziara hiyo ni kuhakikisha kwamba Marekani inaendelea kujikita “kusaidia nchi za Afrika” kwa lengo la kuimarisha ushawishi kila kunapotokea fursa

Inaendelea Uk. 11



Kamala Harris akihutubia mara baada ya kuwasili nchini Ghana jana

Kamala Harris aja kufagilia Marekani



Kamala Harris akiwa nchini Ghana jana

Inatoka Uk. 10

inazoweza kuzidaka katika Afrika kabla ya nchi nyingine, hasa China.

“Upo uwezekano mkubwa kwamba Harris atajadili pia namna Marekani inavyojimarisha kuhakikisha urafiki wake na Afrika hauporwi na China, na hapo anaweza kueleza namna China inavyozibana nchi za Afrika katika kulipa madeni yake tofauti na wao,” anasema Dkt. Lenny Kasoga.

Dkt. Kasoga mbobezi katika siasa na uchumi wa kimataifa na pia mhadhiri wa vyuo vikuu, anasema Marekani imeanza kuhofia uhusiano wa China na Afrika, hivyo lazima itangaze “udugu” wake na Afrika mara kwa mara.

Vyanzo vya uhakika vimeliambia Pambazuko kwamba kiongozi huyo pia katika ziara yake, “ataanika” namna China inavyoweza kuwa “rafiki mbaya” ikitokea nchi imeshindwa kurejesha mikopo yake kwa wakati.

China inadaiwa kuwa nchi iliyokamata baadhi ya uendeshaji wa mashirika na kampuni kwa nchi za Afrika ambazo zilishindwa kulipa madeni yake. Hata hivyo, jambo hili limekuwa likikanushwa na China na kuita “propoganda za kipuuzi.”

Inaelezwa pia Harris huenda akatumia mwanya wa ziara hiyo Tanzania kuzungumza na Rais Samia Suluhu Hassan juu ya kuongeza ushiriki wa wanawake wengi zaidi katika ngazi za umuzi ikiwamo bunge na maeneo mengine.

Msururu wa viongozi wa Marekani kutembelea Afrika au kuwa na mikutano na viongozi wa nchi za bara hilo ni dhahiri baada ya rais wa nchi hiyo tajiri, Joe Biden kuwaalika viongozi wa Afrika Desemba, mwaka jana.

Kama hiyo haitoshi, rais huyo wa Marekani atafanya ziara barani Afrika baadaye mwaka huu.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken naye amekuwa akifanya ziara kadhaa Afrika na mwezi huu alikuwa Ethiopia na Niger, ikiwa ni kipindi kifupi baada ya kuzuru Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Morocco, Algeria na Rwanda.

Rais Biden, anavunja “ukaidi” wa mtangulizi wake, Donald Trump, ambaye kwa kiasi kikubwa alipuuzia uhusiano na nchi za Afrika, kwa kuamini kwamba bara hilo halina lolote la kuisaidia Marekani.

Pambanuo kutoka Marekani

Tanzania ijipange kukabili majanga

Na Godwin Chilewa, Texas, Marekani

ZIPO dalili kedekede zinazoonyesha kuwa Tanzania haijajipanga vyema kukabili dharura au majanga ya kidunia, mojawapo ya dalili hizo ni kutokuwepo kwa akiba kubwa ya mafuta ya kuendesha mitambo.

Wakati nchi zingine zikiwa na akiba ya mafuta kwa miaka miwili – wakati wote, Tanzania inaeleza kuwa na akiba ya miezi miwili tu ya nishati hiyo muhimu.

Nchi kuwa na akiba kidogo ya mafuta, ni hatari sana, kwani kunapotokea majanga ya asili; mafuriko, kimbunga, matetemeko, au hata yale yanayosababishwa na binadamu - kama vile vita, maendeleo wa nchi huwa shakani. Mafuta yakikosekana, hakuna kinachoendelea!

Ni muda muafaka sasa kwa Tanzania kupanga mipango ya kuwa na akiba ya mafuta kwa angalau mwaka mmoja, ili kuhakikisha kuwa kwa kipindi hicho, endapo kutatokea lolote, uchumi wa nchi hautaporomoka na maisha ya watu wake yataendelea.

Mbali na suala la kuhifadhi mafuta ya kutosha ili kujilinda na kuporomoka kwa uchumi, ni wakati muafaka sasa kwa serikali anayoongoza Rais Samia Suluhu Hassan, kubadili mtazamo na mfumo wa kupambana na ufukara wa wananchi.

Rais Samia apangue mifumo aliyoikuta na ajenge yake ambayo siyo tu itaacha alama ya uongozi wake, bali itainua, kuimarisha na kuboresha maisha ya watu anaowaongoza.

Awekeze zaidi mitaji, utaalamu na fursa kwenye miradi ya uzalishaji mali inayosaidia wananchi kuinua kipato chao.

Hivi sasa bado serikali inasuasua kuwa na mikakati ya uwekezaji mkubwa katika kilimo cha mboga, matunda, mazao ya nafaka, na hata mazao ya biashara japokuwa ardhi yenye rutuba iko bwelele.

Hili pengine linatokana na mtazamo uliopo hivi sasa kuwa serikali kazi yake ni kukusanya kodi tu, na siyo kujihusisha



Rais Samia Suluhu Hassan

moja kwa moja na shughuli za kuwekeza katika njia kuu za kuimarisha uchumi.

Hata hivyo, ukiziangalia kwa makini nchi nyingi zilizoendelea, utaona kuwa maendeleo ya kilimo, biashara na viwanda katika nchi hizo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na mikakati ya serikali kuwawezesha wahusika kwa hali na mali.

Hebu juulize kwa nini serikali haiweki kiwanda cha kusindika vinywaji vitokanavyo na mabibo mikoa ya kusini, au sehemu nyingine kunakolimwa zao hilo?

Kwa nini tunashindwa kuwa wauzaji wakubwa wa maparachichi duniani wakati kule Mbeya matunda hayo yanaoza tu? Kwa nini tunaagiza mafuta ya kula nje wakati alizeti, michikichi, minazi, karanga, maparachichi na ufuta vimejazana nchini?

Napenda kusisitiza haja ya viongozi wetu kuwa na maono mapya katika kuliendeleza taifa badala ya kuwa na mawazo mgando ya kufikiria siasa na uchaguzi pekee.

Ng'wanamalundi na miujiza yenye maswali mengi - II

Na Ibengwe Shileki MAZEGE

WIKI iliyopita, tulisoma kwamba siku moja kabla Ngolo hajajifungua mtoto, wingu kubwa lilitanda. Mvua kubwa na yenye radi kali ikaanza kunyesha. Mtoto aliyekuwa tumboni mwa mama yake akaruka “mruko” usio wa kawaida na kisha ikasikika sauti ya kitoto kutoka tumboni ikisema, “máyù nibyalage” (maneno ya Kisukuma; yaani “mama nizae”).

Kusikia maneno hayo, Ngolo akashtuka na kuingiwa hofu, hivyo akamuita mama mkwe wake na baadhi ya majirani ili nao waweze kuwa mashahidi wa sauti hiyo. Kwa bahati nzuri sauti ile ikajirudia tena na ghafla uchungu ukamshika Ngolo.

Hiyo inaeleza kuwa mwishoni mwa mwaka 1892, Ngolo alijifungua mtoto wa kume mwenye maajabu tangu akiwa tumboni mwake. Mtoto huyo akaitwa Igulu, yaani Mbingu.

Igulu (Mwanamalundi) alizaliwa akiwa mwenye afya njema kabisa isipokuwa tu miguu yake ilikuwa myembamba na yenye nyayo kubwa tangu alipozaliwa. Kutokana na wembamba wa miguu yake, jamii ikampa jina la utani “Mamilundi” likimaanisha “mamiguu myembamba”.

Kijana Igulu alikuwa ni mtu mwenye aibu sana enzi za utoto wake. Alikuwa akiwakimbia wageni wasimuone na kuuficha uso wake kwa aibu. Pamoja na aibu alizokuwepo nazo, alipenda sana kuzurura mitaani akiwa ameambatana na marafiki zake.

Baadhi ya ndugu zake, hasa wazazi wa marafiki zake wengi, hawakupendezwa na tabia yake ya uzururaji akiwa ameambatana na watoto wao. Mara kadhaa wazazi wa marafiki wa Igulu walimtambia Igulu (Mwanamalundi) maneno mabaya kila alipotoka kuzurura na wenzake, walimwambia, “Mamirundi galyo lilihumbura bana bise”, ikiwa na



Ng'wanamalundi

maana “ona lenye mamiguu yake marefu linarubuni watoto wetu.”

Katika ujana wake Igulu, alipenda sana kucheza ngoma aina ya Kahela. Kila aliposhiriki kucheza ngoma hiyo, alipenda sana kuuficha uso wake kwa kitambaa cheusi. Katika mashindano ya kucheza ngoma hiyo, Igulu na marafiki zake walishindwa mara kadhaa katika mashindano ya ngoma za Kisukuma.

Igulu na vijana wenzake wakiwa na kikundi chao cha ngo, a walishindwa kufurukuta kwa wacheza ngoma maarufu wa Usukumani kama Samike, Ng'wanikinga, Ng'wanilong'ho na Gindù Nkima. Haikuwa rahisi kuwashinda katika uchezaji wa ngoma. Ni watu ambao walijua kucheza ngoma kwa umahili kuliko Igulu (Mwanamalundi). Mara nyingi wakiaminika kutumia uchawi kuwapa ushindi.

Kutokukubalika kwa Igulu (Mwanamalundi) na marafiki zake mbele ya jamii, hasa katika uchezaji wa ngoma, kulisababisha achukue uamuzi wa kwenda kwa mganga.

Igulu aliwashawishi vijana wenzie waende kwa mganga atakayewapa dawa ya mvuto kwa watu na kuwa washindi nyakati zote za mashindano ya ngoma. Vijana wenzie walikubali sababu kwa nyakati zile suala la kwenda kwa mganga lilikuwa ni jambo dogo sana.

Safari ya kuelekea mashariki zaidi mwa

Watu Maarufu**Ng'wanamalundi na miujiza***Inatoka Uk. 13*

kijiji chao ikawadia. Mganga alikuwa ni mwanamke, mwenye umri ufaao kuitwa bibi ndani ya kijiji cha Nyaraja, Wilaya ya Iramba, Singida. Walipofika, baada ya safari ya kutembea kwa muda mrefu, hatimaye walifika kwa mganga.

Walipokelewa vizuri na mwenyeji wao. Iliwachukua wiki moja bila kuhudumiwa chochote kile, siku ya nane mganga akawaamuru wachukue panga na majembe kuelekea porini ili wakachimbe dawa itakayowasaidia kupendwa na watu.

Wakiwa porini, yule bibi mganga alitafuta vinyonga watatu kwa idadi ya vijana hao wanaotaka dawa, kisha akawaambia wachimbe mashimo yenye nusu ya urefu wao. Vijana wakachimba mashimo hayo huku wakiwa na vinyonga vichwani mwao.

Walipomaliza kuchimba, bibi mganga akawaambia wafunike mashimo hayo kwa kuni kavu. Vijana hao wakatii maagizo ya bibi mganga na kisha bibi akawatoa vinyonga waliokuwa wameng'ang'anua kwenye vichwa vya vijana hao watatu.

Baadaye akawatia dawa midomoni vinyonga hao na kisha akawaweka juu ya kuni zilizofunika mashimo yale yaliyochimbwa na vijana wale watatu. Kisha akawaweka vinyonga hao juu ya kuni zile, moto ukawashwa ili kuwachoma vinyonga hao.

Hazikupita dakika kadhaa wakiwa wanashuhudia kuteketea kwa vinyonga hao, ghafla akatokea kifaruru katika mazingira ya kutatanisha na akaanza kuwafukuza watu wote, akiwemo yule bibi mganga.

Igulu ilimlazimu kupanda juu ya mti kujinusuru na hatari ile. Wale vijana wawili walitimka mbio na hawakurudi tena. Bibi mganga akararuliwa na yule kifaruru mpaka akapoteza maisha na kisha kifaruru akamjia Igulu aliekuwa juu ya mti na kuanza kuushambulia ule mti kwa pembe.

Hata hivyo, kifaruru hakufanikiwa kuuangusha mti aliopanda Igulu zaidi ya kuubandua magome yake. Kifaruru alipochoka akaamua kuondoka na kutokomea kusikojulikana.

Igulu akashuka juu ya ule mti na kumwendea bibi mganga ambaye muda huo alikuwa ni marehemu. Igulu akaubeba mwili wa yule bibi mganga na kuurudisha nyumbani. Akiwa njiani, ule mwili wa bibi mganga uliokuwa mabegani mwake ukaonesha dalili za mtu kupumua.

Ghafla yule bibi akapiga chafya na kuamka kisha akamuuliza Igulu, "bhaja hali abhayanda abhalaha" akimaanisha kuwa wako wapi vijana waliokuwa hapa? Igulu akamwambia kuwa wale vijana wenzie wamekimbia baada ya kumuona yule kifaruru.

Bibi mganga ambaye muda huu alionekana kuwa ni mzima kabisa na hana majeraha tena, akaomba warudi eneo la tukio ili wachukue dawa. Wakiwa njiani kurudi eneo la tukio, yule bibi mganga akamsifia sana Igulu kwa kumuita "Ni mwanaume kamili" aliyekuwa kweli kutafuta dawa. Bibi akaokota yale magome yaliyobanduliwa na kifaruru na kisha kuondoka nayo.

Itaendelea wiki ijayo...**Faru**

Pambazuko

**SASA
TUNAPOKEA
MATANGAZO**

**EWE
MFANYABIASHARA
NA MTOA HUDUMA,
ENDAPO UNAHITAJI
KUWAFIKIA WATEJA
WENGI ZAIDI BILA
KUJALI MIPAKA YA ENEO
ULILOPO, TANGAZA
NASI KWA**

Kuwasiliana kupitia: 0744 768 263
au Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Imani

Dhamana, fedha zisifanye kukufuru

Na **Benedict MSOFFE**,
Vatican

MAFANIKIO makubwa ya binadamu mara nyingi humfanya asahau nafasi yake na kujaribu hata kuchukua nafasi ya Mungu. Matokeo ya kiburi hicho huwa ni kupatwa na mapigo makubwa.

Ufalme maarufu wa Israeli ambao ulipata kutawaliwa na wafalme mashuhuri – wakiwamo Daudi na Solomoni, hatimaye ulipigwa na mpasuko mkubwa uliosababisha mgawanyiko wake mwaka 933 K.K. – na kulizaliwa falme mbili.

Ule wa kaskazini ulioitwa Israeli ukiwa na makao makuu mjini Samaria; na ufalme wa kusini ulioitwa Yuda ukiwa na makao makuu mjini Yerusalemu. Alikuwapo mfalme wa Yuda aliyetitwa Uzia, aliyeshi kati ya miaka 783 – 742 K.K. Alikuwa na umri wa miaka 16 tu alipoutwaa ufalme baada ya baba yake Amazia na aliyetawala Yerusalemu kwa miaka 52.

Mwanzoni Uzia alimcha Mungu na akafanikiwa sana. Utawala wake uliilinda Yuda dhidi ya maadui wote. Uzia akajenga minara, akachimba visima, akalalisha ng'ombe wengi na zabibu mashambani.

Alikuwa na jeshi kubwa, akabuni mitambo ya kivita ya kurusha mishale na mawe makubwa, ikawekwa juu ya minara. Kwa kifupi, Uzia alijijengea heshima kubwa na sifa zake zikaenea kila kona.

“Lakini alipokuwa na nguvu, moyo wake ulitukuka, hata akafanya maovu,

kwani aliingia hekaluni mwa Bwana ili afukize uvumba juu ya madhabahu ya kufukizia” - (2 Nyakati 26: 16).

Katika dunia ya leo ambapo tunachukulia kila kitu kuwa ni sawa tu, tutajiuliza sasa kulikuwa na kosa gani? Lakini Uzia hakuwa Kuhani. Alifikiri kwa sababu ya mafanikio yake makubwa, basi angeweza tu kujitwalia hata mamlaka ya kiroho ambayo Mungu aliyathibitisha kwa namna ya kipekee kwa makuhani kuwekwa wakfu.

Aliona kuwa makuhani hawana maana na yeye angeweza kuifanya kazi yao vizuri zaidi.

Uzia hakujali juu ya ulazima wa kuhani aliyewekwa wakfu kutolea sadaka ile. Kuhani ni mtu ajuaye namna ya kuingia patakatifu na kuchota mema kutoka huko baraka na manufaa ya patakatifu na kuwashirikisha watu bila kupanajisi patakatifu (Walawi 16).

Hata kama alikuwa na akili nyingi, maarifa na mafanikio, Uzia hakujua lolote juu ya namna ya kuenenda katika patakatifu. Kuhani Azaria, pamoja na wenzake 80 wakamsihi sana Mfalme Uzia asikufuru, lakini yeye kwa kiburi akawaka hasira.

Wakati akiwaka hasira, palepale akapatwa na ugonjwa wa ukoma katika paji la uso. Mfalme kwa sababu hiyo alitengwa hadi siku ya kufa kwake na ilimlazimu kumrithisha mwanawe Yothamu ufalme. Mamlaka, nguvu na mafanikio tulivyo navyo leo vinatufanya wajuaji juu ya utakatifu wa Mungu na juu ya patakatifu pake?



Uchambuzi

Wamarekani mamboleo na maadili asilia

Na Dkt. Renatus CARTESIUS

WAMAREKANI wa kizazi cha miaka ya 1960 na kuendelea, wakiongozwa na hayati Profesa Germain Grisez, hawakuridhishwa na dosari kadhaa katika nadharia kongwe ya maadili asilia, ambayo msingi wake ni hoja ifuatayo:


Kwamba, kwa mujibu wa maumbile yao, watu ni viumbe wenye matamano asilia ya kutunza uhai, uzazi, ukweli, urafiki, jumua na malengo mengine yanayohusiana na silika asilia za kimwili na kiakili walizo nazo;

Kwamba, mara zote na katika sehemu zote, viumbehai wote waliomo katika tabaka moja wanapaswa kuenenda katika namna ambayo inaonyesha utii kwa kila silika asilia ya kimwili na kiakili waliyo nayo;

Na kwamba, kwa hiyo, watu wanapaswa kuenenda katika namna ambayo inaonyesha utii kwa silika asilia za kibayolojia walizo nazo, na kujiuzuia kuzikiuka silika hizo.

Mifano ya silika asilia za kibinadamu ni mingi. Kwa upande mmoja, kuna watu wana silika asilia ya kupenda miguu minene kama chupa ya bia (crurophilia), kupenda matiti yaliyotuna (lactophilia), kupenda macho makubwa (oculophilia), kupenda nywele ndefu (tricophilia), kupenda kufanya mapenzi (erotophilia), kupenda umati (agorophilia), kupenda mtu wa jinsia tofauti (heterophilia), kupenda mtu wa jinsia moja (homophilia), kupenda watoto (pedophilia), kupenda wazee (gerontophilia), na silika asilia ya kupenda ugomvi.

Na kwa upande mwingine, kuna watu wana silika asilia ya kuogopa kufanya mapenzi (erotophobia), kuogopa umati (agoraphobia), kuogopa mtu wa jinsia tofauti (heterophobia), kuogopa mtu



Prof. Grisez

wa jinsia moja (homophobia), kuogopa watoto (pedophobia), kuogopa wazee (gerontophobia).

Dosari kubwa ya nadharia kongwe ya maadili asilia ni ukweli kwamba, haitwambii ni “silika asilia” zipi zinapaswa kupewa utii na “silika asilia” gani zinapaswa kukiukwa, lini, wapi na kwa nini.

Mfano, haituelezi kwa nini tabia ya kupenda ugomvi inayotokana na “silika asilia ya hasira” ni tabia mbaya wakati tabia ya kupenda ucheshi inayotokana na “silika asilia ya ucheshi” ni tabia nzuri.

Haituelezi kwa nini uzinzi na uasherati ni tabia mbaya wakati tendo la ndoa ni tabia nzuri, japo matendo yote matatu yanatokana na “silika asilia ya uheterofilia.”

Na haituelezi kwa nini ni kosa kimaadili kuitii “silika asilia ya uheterofilia” wakati ni halali kuitii “silika asilia ya uhomofilia,” japo zote ni “silika asilia.”

Kwa sababu ya dosari hizi, Wamarekani mamboleo waliamua kuyatafsiri upya

Uchambuzi

Wamarekani mamboleo na maadili asilia

Inatoka Uk. 17

maadili asilia kwa kutumia misamiati mipya kwa ajili ya kuunda nadharia mamboleo ya maadili asilia.

Kama ilivyo kwa mifumo yote ya kimaadili, tafsiri yao inatoa majibu kwa maswali makubwa kumi.

Nafupisha majibu yao hapa chini kwa msaada wa fikra za wanazuoni wafuatao: Germain Grisez (1965) na makala yake, "The First Principle of Practical Reason,"; Germain Grisez (1987) na wenzake katika makala yao, "Practical Principles, Moral Truth, and Ultimate Ends"; Patrick Lee and Robert P. George (2008) na kitabu chao, "Body-Self Dualism in Contemporary Ethics and Politics"; John Finnis (2011) na kitabu chake, "Natural Law and Natural Rights"; Chiassoni (2014) na makala yake, "Kelsen on Natural Law Theory"; pamoja na Melissa Moschella (2019) na makala yake, "Sexual Ethics, Human Nature, and the 'New' and 'Old' Natural Law Theories."

Kuhusu swali la kiteolojia

Moja, kuhusu swali la kiteolojia linalouliza, "mpango wa Mungu wa dini yetu unasema nini kuhusu maisha bora na ustawi thabiti wa kila mtu," majibu ya kambi ni haya:

Kwamba, inawezekana kuwa kanuni za maumbile, tunazozikubali kwa kauli moja, zilitoka kwa Mungu fulani, japo hatukubaliani kwa kauli moja ni Mungu yupi amesanifu kanuni zipi, lini na kiviipi;

Kwamba, ubaya wa tabia kama vile wizi hautokani na tamko la kimungu, bali unatokana na ukweli kwamba, tabia hiyo inapingana na kanuni ya ustawi wa watu;

Na kwamba, kwa hiyo, hata bila kujjuliza kanuni za maumbile zimetoka wapi, tunaweza kujadili na kukubaliana kuhusu kanuni za maadili asilia kutokana na kanuni za maumbile pekee bila

kuongelea kanuni za ufunuo wa kimungu.

Jawabu kwa swali la kibayolojia Mbili, kuhusu swali la kibayolojia linalouliza, "binadamu ni kitu chenye hulka ya namna gani endapo udhati wake utatazama kama mti wenye matawi mbalimbali," majibu yao ni haya:

Wanakubali kwamba, wanadamu ni "viumbe wenye miili" yenye kazi kuu mbili, kulinda maisha ya kiumbehai kupitia ushirikiano wa kifiziolojia uliopo kati ya viungo mbalimbali mwilini na kuendeleza ukoo wa watu kwa kuzaa watoto wapya;

Kwamba, wanadamu huzaliwa katika jumua, kukulia katika jumua, na kuunda jumua mpya, na hivyo ni "wanajamii";

Jawabu kwa swali la kisaikolojia Tatu, kuhusu swali la kisaikolojia linalouliza, "kuna uhusiano gani kati ya fikra, uamuzi na matendo ya kibinadamu," majibu yao ni haya:

Kwamba, wanadamu ni "viumbe wenye urazini," yaani uwezo wa kutumia ubongo kufikiri, kukumbuka, kutambua, kuamua na kufanya matendo huru ya kimwili chini ya uongozi wa ubongo, matedo haya yakiwa ni mbinu ya kufanikisha lengo kuu la maisha binafsi na ustawi wa jamii.

Jawabu kwa swali la kiepistemolojia

Nne, kuhusu swali la kiepistemolojia linalouliza, "tunawezaje kupata maarifa kuhusu sifa zinazoambatana na hulka ya ubinadamu na matawi yake anwai," majibu yao ni kama ifuatavyo:

Kwamba, kila mtu mwenye umri wa utu uzima anao uwezo wa kutambua na kutofautisha kati ya tunu zenye mchango chanya na tunu zenye mchango hasi katika ustawi wa binadamu, bila hata

Endelea Uk. 19

Wamarekani mamboleo na maadili asilia

Inatoka Uk. 18

kuwa na elimu ya darasani. Wanaongelea akili ya kuzaliwa nayo kama chimbuko la maarifa kuhusu tunu za kibinadamu.

Wanaendelea kudai kwamba, kanuni za msingi za maadili asilia, zenye kazi ya kutusaidia kutofautisha kati ya matendo mema na matendo mabaya kwa ujumla, huwa na sifa zifuatazo: zinajikaribisha zenyewe kwenye akili ya kila mtu mwenye umri wa kiutu uzima; kwamba hazitokani na mchujo wa kimantiki unaoanzia ama kwenye taarifa zinazoeleza udhati wa kimetafizikia kuhusu maumbile ya binadamu; au kwenye taarifa zinazoeleza udhati wa kisayansi kuhusu maumbile ya binadamu; au kwenye taarifa zinazoeleza udhati wa kiufunuo kupitia misahafu;


Wanafafanua kuwa, hata hivyo, elimu ya darasani katika masomo ya sayansi na falsafa yanao mchango kwa kuwa yanasaidia “kutukumbusha” juu ya mipaka ya sifa zinazoendana na hulka ya ubinadamu.

Jawabu kwa swali la kisemiotiki

Tano, kuhusu swali la kisemiotiki linalouliza, “tunaweza kutumia alama gani za mawasiliano tunapobadilishana maarifa tuliyo nayo juu ya hulka ya ubinadamu,” majibu yao ni haya:

Kwamba, misamiati muhimu katika kujadili kanuni za maadili ni ustawi wa watu, maisha bora, akili timamu, utashi huru, mema ya kibinadamu, mabaya ya kibinadamu, tunu za kibinadamu, na haki za kibinadamu;

Na kwamba, haki za kibinadamu ni mbinu za kivitendo zinazohusiana na utekelezaji wa majukumu chanya yenye sura ya mahimizo, na uzingatiaji wa majukumu hasi yenye sura ya makatazo, kwa ajili ya kukuza na kuhami tunu za kibinadamu, tunu hizo zikiwa ni malengo.



Marcus Cicero

Jawabu kwa swali la kiakisiolojia

Sita, kuhusu swali la kiakisiolojia linalouliza, “maarifa yetu kuhusu sifa zinazoambatana na hulka ya ubinadamu yanaonyesha kwamba ni tunu zipi zenye mchango chanya kwa ustawi wa watu na tunu gani zenye mchango hasi kwa ustawi wa watu,” majibu yao ni haya:

Kwamba, baada ya kupimwa katika mizania ya urazini wa watu, tunu zilizo na mchango chanya katika ustawi wa binadamu (tunu chanya) ni sababu za kuhlalisha tabia za kibinadamu, na tunu zilizo na mchango hasi katika ustawi wa binadamu (tunu hasi) ni sababu za kubatilisha tabia za kibinadamu;

Kwamba, kama tunu chanya zikiwekwa sambamba na tunu hasi tunapata jozi zifuatazo za tunu:

Kuna umaskini dhidi ya utajiri, uhuru dhidi ya utumwa, njaa dhidi ya shibe, raha dhidi ya mateso, uhai dhidi ya kifo, ujamaa dhidi ya upweke, umoja dhidi ya utengano, maarifa dhidi ya ujinga,

Uchambuzi

Wamarekani mamboleo na maadili asilia

Inatoka Uk. 19

ukweli dhidi ya uwongo, mazoezi ya kimwili dhidi ya kubweteka, urafiki dhidi ya uadui, ujirani mwema dhidi ya ujirani mbaya, umoja kati ya mwili na roho dhidi ya uhasama kati ya mwili na roho, umoja kati ya mawazo na matendo yako dhidi ya mpasuko kati ya mawazo na matendo yako, na kufuata mpango wa Mungu wako dhidi ya kukaidi mpango wa Mungu wako.

Kwamba, kuna tunu za msingi na tunu saidizi, ambapo tunu saidizi ni mbinu za kuzifikia tunu za msingi. Mfano, wanaongelea tunu za msingi, kama vile uhai, dhidi ya tunu saidizi, kama vile shibe.

Jawabu kwa swali la kiprakisiojia


Saba, kuhusu swali la kiprakisiojia linalouliza, “tunawezaje kupangilia malengo, mbinu, na mazingira ya utekelezaji ili kupata ufanisi wa matokeo yanayotakiwa,” majibu ya kambi ni haya:

Kwamba, kila kitendo cha kibinadamu ni mbinu inayotekelezwa kwa ajili ya kufanikisha lengo fulani, na katika mazingira fulani, mazingira hayo yakiwa yanatueleza ulini, uwapi, na uvipi wa kitendo husika.

Mfano, huwa tunawasha moto (lengo) kwa kutumia njiti ya na kasha kavu la kiberiti (mbinu) ndani ya chumba kisicho na upepo mkali (mazingira), kwa kuwa kuna muungano wa lazima wenye sura ya kietiolojia , yaani sura ya sababu na matokeo, kati ya vitu hivi vitatu.

Jawabu kwa swali la kimaadili

Nane, kuhusu swali la majukumu ya kimaadili linalouliza, “maarifa yetu kuhusu sifa zinazoambatana na hulka ya ubinadamu yanaonyesha kwamba ni mbinu zipi zenye mchango chanya



Thomas Hobbes

kwa ustawi wake na mbinu gani zenye mchango hasi kwa ustawi wake,” majibu yao ni haya:

Kwamba, kanuni za maadili ni miongozo kuhusu matendo yanayotakiwa kwa ajili ya kufanikisha ustawi wa kiumbehai, kama vile binadamu, kulingana na hulka yake ya kimaumbile;

Kwamba, hulka ya ubinadamu inabainisha tunu za msingi na tunu saidizi, zote zikiwa muhimu kwa ustawi wa watu;

Kwamba, kila mtu anaweza kufika katika kilele cha mlima wa “maisha bora” endapo, kila tendo analolifanya kwa makusudi litaheshimu tunu zote za msingi, kwani kila tunu ya msingi inao mchango chanya katika ustawi wake.

Na kwamba, kwa hiyo, kutokana na dokezo la kwanza na dokezo la pili hapo juu, inafuata kimantiki kwamba, tunu za msingi zinapaswa kuheshimiwa

Wamarekani mamboleo na maadili asilia

Inatoka Uk. 20

na kila mtu, kila wakati, na kila mahali. Yaani, taarifa zinazohusiana na tunu ndio chimbuko la majukumu yote ya kimaadili.

Jawabu kwa swali la kimantiki

Tisa, kuhusu swali la mchujo wa kimantiki linalouliza, “tunawezaje kuchuja na kupata kanuni za kimaadili kutokana na maarifa yetu kuhusu sifa zinazoambatana na hulka ya ubinadamu, lakini bila kuvunja kanuni za kimantiki,” majibu yao ni kama ifuatavyo:

Kwamba, kanuni muhimu ya kufanya mchujo wa kimantiki kuanzia kwenye madokezo kuelekea kwenye hitimisho, inasema kuwa, taarifa zote zilizo kwenye hitimisho lazima zitokane na taarifa zilizo kwenye madokezo;

Kwamba, taarifa zinazobebwa na kanuni za kimaumbile zinaongelea hali ya mambo yalivyo, au hali ya mambo yanavyopaswa kuwa, bila kujali kama binadamu anataka au hataki hali hiyo itokee; wakati taarifa zinazobebwa na kanuni za kimaadili zinaongelea matendo yanavyopaswa kufanywa au kutofanywa na binadamu kwa kuzingatia hiari ya kimaamuzi ya binadamu huyo;

Kwamba, kwa hiyo, taarifa za kimaadili zilizo kwenye hitimisho la hoja yoyote haziwezi, na hazipaswi, kutokana na taarifa za kimaumbile zilizo kwenye madokezo ya hoja husika, kwani kufanya hivyo ni sawa na kuvuna mchicha kutoka katika shamba la bangi.

Badala yake, wanasema kuwa, taarifa za kimaadili zilizo kwenye hitimisho la hoja yoyote zinapaswa kutokana na kanuni za kipraksiolojia, yaani “praxiological ought-statements.”

Kanuni hizi hueleza uhusiano wenye sura ya kietiolojia, yaani sura ya sababu na matokeo, kati ya matendo ya binadamu

na tunu zinazohusiana na ustawi wa watu, kulingana na maumbile yao kama tabaka la viumbehai wenye mwili, akili na utashi huru.

Hata hivyo, mtazamo huu unakumbana na changamoto moja kuhusu orodha kamili ya “tunu zinazohusiana na ustawi wa watu.” Watu tofauti katika mapokeo tofauti wanatengeza orodha tofauti.

Swali linalohusu falsafa matumizi

Na kumi, ni swali linalohusu falsafa matumizi, yaani namna ya kutofautisha matumizi ya majawabu ya maswali haya nane katika sekta tofauti za maisha ya watu.

Kama tukitumia mfano wa sekta ya “afya ya mama na mtoto,” majibu ya kambi hii ni kama ifuatavyo: Kwamba, kwa kuwa lishe sio tunu ya msingi, sio kosa kila wakati, kila mahali, na kwa mama anayenyonyesha kukamua na kumwaga maziwa yaliyo katika matiti yake, hasa kama hakuna uwezekano wa kumpata na kumyonyesha mtoto wake kwa wakati huo.

Na kama tukitumia mfano wa “vinyweleo na kazi yake ya kuupoza mwili,” majibu ya kambi hii ni kama ifuatavyo: Kwamba, kuwa kupoza mwili kwa njia ya jasho sio tunu ya msingi, basi, sio kosa kila wakati, kila mahali, na kwa kila mhusika kutumia pafyumu zinazositisha kazi ya kutoa jasho mwilini, hasa kama yuko katika mazingira ambako jasho litamkwaza.

Mifano hii miwili inaendana na uhalisia wa maisha ya kila siku.

Majumuisho ya makala

Kwa kuhitimisha, kutokana na pendekezo linalotofautisha kati ya tunu za msingi na tunu saidizi, Wamarekani

Uchambuzi

Wamarekani mamboleo na maadili asilia

Inatoka Uk. 21

mamboleo wameweza kutegua vitendawili vifuatavyo:

Nadharia yao inatueleza kwa nini ni kosa kimaadili kwa mtu kuitii “silika asilia ya hasira” aliyo nayo kwa kuwapiga wenzake. Sababu yao ni kwamba, kitendo hicho kinajeruhi tunu ya urafiki.

Inatueleza kwa nini ni kosa kimaadili kwa mwanamume mwenye “silika asilia ya kujamiiana na mwanamke” kuitii “silika” yake kwa kufanya mapenzi na mtu asiye mke wake, wakati tendo hilo hilo ni halali kimaadili kama akilifanya pamoja na mkewe. Sababu yao ni kwamba, kitendo hicho kinadhoofisha tunu ya ndoa ya jinsia tofauti.

Inatueleza kwa nini ni kosa kimaadili kwa mwanamume mwenye “silika asilia ya kufanya ulawiti” kuitii “silika” yake kwa kumlawiti mwanaume mwenzake. Sababu yao ni kwamba, kitendo hicho ni sawa na kudharau tunu ya ndoa ya jinsia tofauti.

Na inatueleza ni zipi “silika asilia za kibayolojia” zinapaswa kupewa utii na kila mtu, kila mahali na kila wakati; na silika zipi zinaweza kukaidiwa na kuminywa ama kwa muda, au kwa sehemu au kwa ujumla.

Jawabu lao ni kwamba, silika zinazohusiana na tunu za msingi zinapaswa kupewa utii na kila mtu, kila mahali na kila wakati.

Lakini, pamoja na maboresho haya, bado kambi hii haijajipambanua vizuri kuhusu mambo kadhaa.

Mosi, ni kuhusu orodha kamili ya tunu za msingi. Kulingana na mapokeo yake, kila mhusika ndani ya kambi hii anataja orodha yake ya tunu, tena orodha ambazo zinaacha milango wazi kuhusu uwezekano wa kuongezeka.

Pili, kambi hii haina maelezo kamili



Aristotle

kuhusu vigezo wanavyotumia kuziweka tunu zilizo tofauti katika kundi moja. Mfano, uhai wa gameti (tunu saidizi) na uhai wa mimba ambayo ni binadamu mpya (tunu ya msingi) inaunganishwa na kuongelewa kama tunu moja.

Tatu, kambi hii haiaminiki katika msimamo wake kwamba tunu zote za kibinadamu zinaweza kugunduliwa na mtu yeyote mwenye akili timamu za kiutu uzima, pasipo mafunzo rasmi.

Na nne, kambi hii haina maelezo ya kutosha kuhusu lini baadhi ya tunu za msingi zinapaswa kuchukuliwa kama tunu saidizi, na kinyume chake.

Mfano mzuri wa utata huu ni kuhusu tunu kama vile afya, ndoa, uhai, na “umoja wa kimwili na kiroho” ambazo kuna wakati ni tunu za msingi na wakati mwingine tunu saidizi.

Makala inayoajadili “Maadili asilia katika mtazamo wa Waafrika” itaonyesha jinsi Waafrika mamboleo wanavyopendekeza kumaliza dosari hizi.

Haller aifunga saratani 1-0

MCHEZAJI wa timu ya soka ya Borussia Dortmund ya Ujerumani, Sebastien Haller ametagaza kupona kabisa saratani ya korodani.

Haller ambaye pia ni mchezaji wa timu ya taifa ya Ivory Coast, amesema atatumia “bahati ya kupona kwake” kuwatia moyo watu wote wanaougua ugonjwa huo na kuhimiza kuamini uchunguzi wa mara kwa mara – na mapema. Pia matumizi ya tiba sahihi endapo mtu atagundulika kuwa na ugonjwa huo.

“Nilipopata taarifa ya kuugua saratani, kitu cha kwanza kichwani kilikuwa ni kifo, nilikuwa natambua kwamba ukipata ugonjwa huo, tayari umekata tiketi ya kwenda kaburini, lakini nikatiwa moyo na ndugu, jamaa na hata madaktari, kwamba naweza kupona kabisa,” alisema Haller.

Haller anasema, kwa kupona saratani (kansa), ameushinda ugonjwa huo kwa bao 1-0.

Haller aligundulika kuwa na saratani ya korodani muda mfupi baada ya kujiunga na Borussia Dortmund kutoka Ajax Julai 2022.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alifanyiwa upasuaji mara mbili na matibabu ya kemikali katika miezi iliyofuata, kabla ya kuanza tiba nyingine ya mionzi ambayo hatimaye ilimpa afueni na baadaye kutangazwa na madaktari kwamba amepona kabisa.

Haller alirejea uwanjani na kuichezea timu yake mechi dhidi ya Augsburg ambapo Borussia ilishinda mabao 4-3. Mchezaji huyo alicheza kwa dakika 28.

Chanzo cha saratani hiyo

Saratani ya korodani ni ugonjwa ambao unaweza kuanzia kwenye moja ya kokwa – au zote za via vya uzazi kwa mwanaume.

Inaelezwa na wataalamu wa afya kwamba saratani ya korodani inawapata zaidi wanaume wenye miaka 20 mpaka 35.

Nitajuaje kama nina kansa ya korodani?

Mwone daktari kama una maumivu kwenye korodani moja au zote, kama una uvimbe kwenye kokwa, au kama unaona kwako zimekuwa nyekundu au zimevimba.

Saratani ya korodani inatibiwaje?

Unaweza kuhitaji upasuaji ili kuondoa korodani zenye saratani. Kama saratani imesambaa kuelekea maeneo mengine ya mwili, unaweza kuhitaji kufanyiwa uchunguzi na baadaye kuanza tiba ya mionzi, tiba kemikali, au kufanyiwa upasuaji zaidi.

Upasuaji ni njia bora zaidi kama saratani imegundulika mapema kabla haijasambaa. Hata kama saratani imesambaa, kuna uwezekano mkubwa kuwa kupona.

Njia rahisi ya kujichunguza mwenyewe endapo una saratani ya korodani ni kuweka dole gumba juu ya korodani na kidole cha chanda na cha kwanza kwa chini. Zungusha korodani katikati ya gumba na vidole mara kadhaa. Rudia pia kwenye korodani nyingine.

Ukihiisi maumivu makali, na yanayodumu kwa muda mrefu, unashauriwa kwenda hospitali kwa uchunguzi zaidi.



Sebastien Haller

MANDONGA TENA...



Bondia wa Tanzania, Karim Mandonga, ameendelea kuonyesha ubabe wake kwenye ndondi baada ya kumchakaza mpinzani wake kutoka Uganda, Kenneth Lukyamuzi katika pambano lililofanyika usiku wa kuamkia jana jijini Nairobi, Kenya. Pambano hilo la raundi nane, lilimalizika kwa majaji kumpa ushindi wa pointi Mandonga na kutangazwa kuwa bingwa wa PST kwa uzani wa Light Heavyweight ikiwa ni ubingwa wake wa kwanza tangu aingie kwenye masumbwi miaka saba iliyopita.

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

